## HALMASHAURI YA WILAYA YA MOMBA

## KUMBUKUMBU ZA KIKAO CHA DHARURA CHA KAMATI YA FEDHA, MIPANGO NA UONGOZI KILICHOFANYIKA TAREHE 27/10/2021 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MOMBA

**MAHUDHURIO:**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA:**

1. Mhe. Mathew M.Chikoti -Diwani Kata ya Mkulwe -M/Kiti H/Wilaya
2. Mhe. Njavwa J.Siame -Diwani Kata ya Nkangamo - M/M/MKiti
3. Mhe. Erick C.Mkamba -Diwani Kata ya Ivuna -Mjumbe
4. Mhe. Kyalambwene Kakwale -Diwani Kata ya Kamsamba -Mjumbe
5. Mhe.Shadrack B.Simfukwe -Diwani Kata ya Kapele -Mjumbe
6. Mhe.Mary M.Siwale -Diwani Viti Maalum - Mjumbe
7. Bi. Regina L. Bieda -Mkurugenzi Mtendaji (W) -Katibu

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA:**

1. Mhe. Condester M.Sichalwe (MB) - Jimbo la Momba

**WATAALAM WALIOKUWEPO:**

1. Bi.Gama E. Z - Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)
2. Bi. Atuganile Fred - Afisa Utumishi (W)
3. Bw. Zhenas Mapunda - Kaimu Afisa Elimu Sekondari (W)
4. Bw. Jofrey Mwambasi - Kaimu Afisa Mipango (W)
5. Bw. Charles Milinga - Kaimu Mkaguzi wa Ndani (W)
6. Bw. Deogratius Mlondela - Kaimu Mweka Hazina (W)
7. Dr. Amani Kilemile -Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
8. Eng. Maria Nsonga -Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W)
9. Bw. Kastom Mgulla -Kaimu Afisa Elimu Msingi (W)
10. Bw. Joseph Mbogela -Kaimu Afisa Nyuki (W)
11. Bw. Peter Mpangala - Kaimu Mganga Mkuu (W)
12. Bi. Hildegarda Kiria - Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii (W)
13. Bw. Mwinyi Yunus -Mwanasheria
14. Bw. Said Mtatula -Kaimu Afisa Ugavi (W)
15. Bw. Bahati Paul - Kaimu Afisa Ardhi na Maliasili (W)
16. Bi. Helen Charles - Kaimu Afisa Kilimo na Umwagiliaji (W)

**WATAALAM WASIOHUDHURIA:**

1. Bw.Alfred Simpoli - Kaimu Afisa Habari na Uhusiano (W)
2. Bw. Miled Maselo - Kaimu Afisa Usafi na Mazingira (W)

**SEKRETARIETI:**

1. Bi.Hazina M. Msongole - Mwandishi wa Vikao vya H/Wilaya

**MUHT.NA.FMU/MOMBA/01/10/2021 AGENDA ZA KIKAO**

Agenda zifuatazo ziliwasilishwa kwa wajumbe kuwa agenda za kikao cha dharura cha Kamati ya Fedha, Mipango na Uongozi cha tarehe 27/10/2021.

1. Kufungua kikao
2. Kuridhia agenda
3. Taarifa ya ujenzi wa Shule za Msingi (Shule shikizi), Sekondari na nyumba za Watumishi wa Afya
4. Taarifa ya mapokezi ya fedha ya miradi ya WASH, ukamilishaji vyumba vya madarasa, mradi wa SWASH na uwekaji wa miundombinu ya maji
5. Kufunga kikao

**MUHT.NA. FMU /MOMBA/02/10/2021 KUFUNGUA KIKAO**

Kabla ya kufungua kikao, Mwenyekiti aliwashukuru Wajumbe kwa mahudhurio. Alisema hiki ni kikao cha dharura kwaajili ya ujenzi wa Shule za Msingi (Shule shikizi), Sekondari na nyumba za Watumishi wa Afya. Alisema Serikali imetoa fedha kiasi cha Sh. 1,830,000,000/= kwaajili ya miradi ya ujenzi ya Elimu na Afya. Alitoa pongezi kwa kazi ya LAAC iliyofanyika kwani taarifa iliandaliwa vizuri alimpongeza Jofrey Mwambasi aliye mwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya kwa uwasilishaji mzuri wa taarifa. Alishauri wataalam wawe wawazi katika kufanya kazi na wawe na ushirikiano, pia alisema mapato yakusanywe ipasavyo.

Baada ya maelezo hayo, Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 04:22 Asubuhi.

**MUHT.NA. FMU /MOMBA/03/10/2021 KURIDHIA AGENDA**

Wajumbe walisoma na kuridhia agenda zilizoandaliwa.

**MUHT.NA. FMU /MOMBA/04/10/2021 TAARIFA YA UJENZI WA SHULE ZA MSINGI (SHULE SHIKIZI), SEKONDARI NA NYUMBA ZA WATUMISHI WA AFYA**

Halmashauri ya Wilaya ya Momba katika Robo ya Pili (Mwezi Oktoba) ya mwaka wa fedha 2021/2022 imepokea barua yenye Kumb.Na.DA.83/127/01/31 ya tarehe 15.10.2021 kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe yenye maelekezo ya Mhe. Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI kuhusu fedha zilizopokelewa kiasi cha shilingi 1,830,000,000.00 kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya Ujenzi wa Vyumba vya madarasa katika shule za Msingi (Shule shikizi), Shule za Sekondari na Nyumba za watumishi wa afya (3 in 1)

**MAPOKEZI YA FEDHA**

Halmashauri ya Wilaya ya Momba tayari imepokea fedha kiasi cha shilingi 1,740,000,000.00 kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 87 vya madarasa ikiwa shule za msingi (Shule shikizi) vyumba 38 vya madarasa sawa na kiasi cha shilingi 760,000,000.00 (Ujenzi wa chumba 1 na uwekaji wa madawati shilingi 20,000,000) na Shule za Sekondari vyumba 49 vya madarasa sawa na kiasi cha shilingi 980,000,000.00 (Ujenzi wa chumba 1 na uwekaji wa madawati shilingi 20,000,000).

Fedha hizi zimepokelewa moja kwa moja katika akaunti za shule kama inavyoonyesha kwenye Mgawanyo katika jedwali hapa chini: -

**Jedwali Na.01.Mapokezi ya fedha za Ujenzi wa vyumba 38 vya madarasa shule za Msingi (Shule shikizi)**

| Na | Shule Mama | Akaunti Namba | Jina la Akaunti | Shule Shikizi | Idadi ya Vyumba vitakavy ojengwa | Kiasi | Jumla ya Fedha |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | CHIPUMPU | 6123700334 | NMB TUNDUMA | MBUTU | 2 | 20,000,000 | 40,000,000 |
| 2 | SENGA | 6123700398 | NMB TUNDUMA | MCHANGANI | 8 | 20,000,000 | 160,000,000 |
| 3 | SAMANG'OMBE | 6123700347 | NMB TUNDUMA | MANG'ULA | 2 | 20,000,000 | 40,000,000 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | NZOKA | 6123700328 | NMB TUNDUMA | MAJENGO | 2 | 20,000,000 | 40,000,000 |
| 5 | NAMING'ONGO | 6123700253 | NMB TUNDUMA | NACHISITU | 5 | 20,000,000 | 100,000,000 |
| 6 | NAMCHINKA | 6123700311 | NMB TUNDUMA | KAPONZYA | 2 | 20,000,000 | 40,000,000 |
| 7 | MPUI | 6123700343 | NMB TUNDUMA | MSUNGO | 2 | 20,000,000 | 40,000,000 |
| 8 | MASANYINTA | 6123700368 | NMB TUNDUMA | MAZINDE | 2 | 20,000,000 | 40,000,000 |
| 9 | LWATWE | 6123700241 | NMB TUNDUMA | MBAMBILA | 2 | 20,000,000 | 40,000,000 |
| 10 | LWATWE | 6123700241 | NMB TUNDUMA | INUNKA | 3 | 20,000,000 | 60,000,000 |
| 11 | KAPELE | 6123700337 | NMB TUNDUMA | NAKATANDUL A | 2 | 20,000,000 | 40,000,000 |
| 12 | IYENDWE | 6123700294 | NMB TUNDUMA | MANGWELE | 2 | 20,000,000 | 40,000,000 |
| 1[illegible] | IVUNA | 6123700227 | NMB TUNDUMA | IKONJE | 2 | 20,000,000 | 40,000,000 |
| 14 | CHINDI | 6123700213 | NMB TUNDUMA | MERU | 2 | 20,000,000 | 40,000,000 |
| | | | | JUMLA | 38 | | 760,000,000 |

**Jedwali Na.02 Mapokezi ya Fedha za Ujenzi wa Vyumba 49 vya Madarasa Shule za Sekondari**

| Na | Shule | Akaunti Namba | Jina la Akaunti | Idadi ya Vyumba vitakavy | Kiasi | Jumla ya Fedha |
|---|---|---|---|---|---|---|

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | ojengwa | | |
| | NZOKA | 61510016435 | NMB TUNDUMA | 4 | 20,000,000 | 80,000,000 |
| 2 | NKANGAMO | 61201100059 | NMB MBOZI | 3 | 20,000,000 | 60,000,000 |
| 3 | CHIKANAMLILO | 61201100029 | NMB MBOZI | 4 | 20,000,000 | 80,000,000 |
| 4 | MOMBA | 61201100038 | NMB MBOZI | 4 | 20,000,000 | 80,000,000 |
| 5 | MSANGANO | 61201100045 | NMB MBOZI | 4 | 20,000,000 | 80,000,000 |
| 6 | MKULWE | 61201100027 | NMB MBOZI | 4 | 20,000,000 | 80,000,000 |
| 7 | MKOMBA | 6121100088 | NMB | 6 | 20,000,000 | 120,000,000 |
| 8 | KAPELE | 61201100072 | NMB MBOZI | 4 | 20,000,000 | 80,000,000 |
| 9 | UWANDA | 61201100080 | NMB MBOZI | 4 | 20,000,000 | 80,000,000 |
| 10 | IVUNA | 61201100088 | NMB MBOZI | 4 | 20,000,000 | 80,000,000 |
| 11 | CHITETE | 61201100054 | NMB MBOZI | 4 | 20,000,000 | 80,000,000 |
| 12 | CHILULUMO | 61510016501 | NMB MBOZI | 4 | 20,000,000 | 80,000,000 |
| | **JUMLA** | | | **49** | | **980,000,000** |

Aidha fedha kiasi cha shilingi 90,000,000 inasubiriwa kupokelewa kwa ajili ya ujenzi wanyumba za watumishi wa Afya yaani 3 in 1

**UTEKELEZAJI WA MRADI**

**HATUA ZA AWALI**

Katika kutekeleza mradi huu wa ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za Msingi, Sekondari na ujenzi wa nyumba za watumishi wa afya 3 in 1 Halmashauri

itazingatia hatua mbalimbali za utekelezaji kwa njia ya Force Account.Hatua zitakazofuata ni kama ifuatavyo:-

I. Kufanya maandalizi ya awali kama vile kuzielekeza bodi za Shule za Sekondari, Kamati za Shule za Msingi pamoja na bodi za Afya kuunda kamati za usimamizi wa miradi

II. Kuhamasisha jamii ili kuweza kuchangia katika miradi hii ya ujenzi ikiwa ni pamoja na Mchanga,Kokoto,Mawe,Kuchimba Msingi, Maji na Matofali

III. Kuandaa wazabuni kwa ajili ya huduma na vifaa kwa kuzingatia kanuni za manunuzi

IV. Halmashauri imeunda kamati ya ufuatiliaji na usimamizi wa mradi ambao ni Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya, Afisa Mipango wa Wilaya, Mwanasheria wa Wilaya, Mweka Hazina wa Wilaya, Afisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya, Mkaguzi wa Ndani wa Wilaya, Afisa Mifugo wa Wilaya, Mganga Mkuu wa Wilaya, Afisa manunuzi wa Wilaya, Afisa Elimu Sekondari, Mhandisi wa Ujenzi wa Wilaya. Aidha timu zingine zitaundwa katika ngazi ya Tarafa, Kata na Kijiji

V. Halmashauri itatoa matangazo ya kazi kupitia tovuti ya Halmashauri ya Momba www.mombadc.go.tz na maeneo yote yenye kuweka uwazi kwa lengo la kupata mafundi wenye ubora na wa bei nafuu

VI. Mabadiliko ya maeneo ya ujenzi yanatakiwa kutolewa taarifa katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na OR TAMISEMI. Pia Halmashauri itachukua picha ya maeneo yote ya ujenzi kabla ya kuanza

**UZINGATIAJI WA UBORA, VIWANGO NA THAMANI YA FEDHA**

Katika kuhakikisha mradi huu unakuwa bora na thamani ya fedha, Halmashauri inapaswa kufanya yafuatayo:-

a. Halmashauri imeandaa Orodha ya vifaa vya ujenzi (Schedule of Material) kwaajili ya kupeleka katika maeneo yote ya utekelezaji wa mradi (Shule za Msingi na Sekondari)

b. Halmashauri imeanza kufanya uhamasishaji kwa jamii juu ya uchangiaji wa mradi ikiwa ni Pamoja na ukusanyaji wa mchanga, mawe na matofali. Uhamasishaji huu umeanza kwa watalaamu wa ngazi za kata na vijiji na waheshimiwa madiwani

c. Halmashauri itakuwa na mpango kazi wa utekelezaji wa mradi (Schedule of work)

d. Halmashauri itasimamia sheria, kanuni na taratibu katika kuhakikisha vifaa vya ujenzi vinavyo nunuliwa vinakuwa bora na kuakisi thamani ya fedha. Kitengo cha manunuzi kwa kushirikiana na Idara itahakikisha Sheria, kanuni na taratibu za manunuzi zinafuatwa

**MUDA WA UTEKELEZAJI**

Fedha zilizopokelewa hazikuwa katika mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022,hivyo Halmashauri inahitaji idhini ya vikao vya wakuu wa Idara (CMT) na Kamati ya Fedha, Mipango na Uongozi kwa ajili ya kuridhia matumizi ya fedha hizi. Kupitia vikao hivi Halmashauri itafanya uhamisho wa bajeti kupitia mfumo wa uandaaji wa mipango na bajeti (PlanRep web based-Reallocation Between Votes) kwa ajili ya kupata idhini ya matumizi ngazi za Shule na vituo vya kutolea huduma za Afya. Mradi huu unategemea kukamilika kwa kipindi cha miezi 3 kuanzia mwezi Oktoba hadi Desemba, 2021 ili kuwezesha uwepo wa vyumba vya madarasa kwa watakaochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2022.

Baada ya mawasilisho ya taarifa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya alishauri yafuatayo:-

a) Kuhusu kuongeza mtumishi wa Idara ya manunuzi kwamba aajiriwe kibarua kwa mkataba kwa kuwa kitengo kina watumishi wachache na miradi ni mingi

b) Kwamba Halmashauri inunue vifaa kwa ujumla kwa majengo yote kwa bei ya kiwandani

c) Kwamba Wananchi waendelee kujitolea nguvu zao kama vile kukusanya Mawe, Kokoto, Mchanga nk

d) Kwamba Madiwani waisimamie miradi inayotekelezwa kwenye maeneo yao

e) Kwamba Madiwani wasaidie kuwatafuta mafundi wazuri na wenyeji wa eneo husika

f) Aliishukuru Serikali kwa kutupatia fedha kwaajili ya miradi ya Elimu na Afya

**Mjadala:**

i. Mhe.M.M.Siwale Diwani Viti Maalum alitaka kujua Shule ya Msingi Mkomba imeingiziwa fedha kwenye akaunti ipi? Pia alitoa ombi kwamba shule mama zina hali mbaya sana fedha zilizotolewa zitumike kukarabati majengo hayo.

- Ilijibiwa kwamba fedha za shule ya Msingi mkomba imeingiziwa fedha kwenye akaunti ya Mpapa kiasi cha Sh. 40,000,000/=
- Katibu Tawala wa Wilaya alieleza kuhusu fedha zilizotolewa kwa miradi ya ujenzi wa shule kwamba fedha zinatakiwa zitumike kwa kuanza na ujenzi wa msingi hatimaye jengo liishe na madawati yanunuliwe na siyo kukarabati majengo ya zamani na alieleza kwamba fedha hizo zinatakiwa zitumike kufikia mwezi Disemba 2021 na mwezi Januari watoto watumie majengo hayo hata hivyo alishauri kwamba mafundi waitwe ili wawe na bei moja kwa kila jengo wasitofautiane

ii. Mhe.E.C.Mkamba Diwani wa Kata ya Ivuna alishauri eneo la ujenzi wa shule shikizi Mchangani, Kazinde na Mang'ula litafutwe eneo lingine kwani lililopo linazingirwa na maji alishauri kamati ifanye ziara kwaajili ya kuona maeneo hayo na kutoa ushauri. Wajumbe waliunga mkono ushauri huo

iii. Mhe.E.C.Mkamba Diwani wa Kata ya Ivuna alishauri kupunguza vyumba vya madarasa katika shule shikizi ya Mchangani na kuvipeleka katika kijiji cha Chuo kwaajili ya kuanzisha ujenzi wa vyumba vya madarasa

- Mhe.M.M.Siwale Diwani Viti Maalum alishauri vyumba vya madarasa 8 katika shule shikizi ya Mchangani vipunguzwe vyumba 4 vibaki mchangani na vingine 4 vipelekwe Chuo.
- Katibu Tawala wa Wilaya alishauri kwamba Afisa Elimu Msingi wa Wilaya awasilishe barua ya matumizi ya fedha kutoka shule yenye madarasa 8 kupunguza na kuyapeleka Chuo

**Azimio:**

i. Wajumbe walikubaliana kwamba kamati ifanye ziara kwaajili ya kuona maeneo ya Mchangani, Kazinde na Mang'ula na kutoa ushauri.

ii. Wajumbe walikubaliana kwamba vyumba vya madarasa 8 katika shule shikizi ya Mchangani vipunguzwe vyumba 4 vibaki mchangani na vingine 4 vipelekwe Chuo.

Wajumbe kwa pamoja waliridhia na kupitisha taarifa ya ujenzi wa Shule za Msingi (Shule shikizi), Sekondari na nyumba za Watumishi wa Afya

**MUHT.NA. FMU /MOMBA/06/10/2021 TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA YA MIRADI YA WASH, UKAMILISHAJI VYUMBA VYA MADARASA, MRADI WA SWASH NA UWEKAJI WA MIUNDOMBINU YA MAJI**

Taarifa ya mapokezi ya fedha ya miradi ya WASH, ukamilishaji vyumba vya madarasa, mradi wa SWASH na uwekaji wa miundombinu ya maji. Iliwasilishwa kwa wajumbe na kupokelewa kama ifuatavyo:-

**MRADI WA WASH:**

i. Ujenzi wa vyoo bora zahanati ya Chitete Sh. 26,700,000/=
ii. Ujenzi wa vyoo bora zahanati ya Nkala Sh. 30,000,000/=
iii. Ujenzi wa vyoo bora zahanati ya Kasinde Sh. 31,000,000/=
iv. Ujenzi wa vyoo bora zahanati ya Nkangamo Sh. 30,000,000/=

v. Ujenzi wa vyoo bora zahanati ya Nzoka Sh. 35,000,000/=
vi. Ujenzi wa vyoo bora zahanati ya Mkutano Sh. 31,559,000/=
vii. Ujenzi wa vyoo bora zahanati ya Myunga Sh. 40,000,000/=
viii. Ujenzi wa vyoo bora zahanati ya Ikana Sh. 30,000,000/=
ix. Ujenzi wa vyoo bora zahanati ya Nyenjele Sh. 35,000,000/=

**UKAMILISHAJI VYUMBA VYA MADARASA**

1. Ukamilishaji wa chumba 1 cha Darasa Mpapa Sekondari 12,500,000/=
2. Ukamilishaji wa chumba 2 vya madarasa Shule ya Sekondari Mkomba 25,000,000/=

**MRADI WA SWASH**

i. Ujenzi wa Choo bora shule ya msingi Mkonko Sh. 6,600,000/=
ii. Ujenzi wa Choo bora shule ya msingi Yala Sh. 6,600,000/=
iii. Ujenzi wa Choo bora shule ya msingi Lozi Sh. 6,600,000/=
iv. Ujenzi wa Choo bora shule ya msingi Nkangamo Sh. 6,600,000/=
v. Ujenzi wa Choo bora shule ya msingi Msangano Sh. 6,600,000/=
vi. Ujenzi wa Choo bora shule ya msingi Chisitu Sh. 6,600,000/=

**UWEKAJI WA MIUNDOMBINU YA MAJI**

1. Kuweka miundombinu ya maji Shule ya Sekondari Msangano Sh. 11,872,379.85/=
2. Kuweka miundombinu ya maji Shule ya Msingi Chuo Sh. 11,872,379.85/=
3. Kuweka miundombinu ya maji Shule ya Msingi Namchinka Sh. 11,872,379.85/=

**MUHT.NA. FMU /MOMBA/07/10/2021 KUFUNGA KIKAO**

Kabla ya kufunga kikao, Mwenyekiti aliwashukuru Wajumbe kwa majadiliano, alisisitiza wananchi wahimizwe kufanya shughuli za maendeleo
Aliwatakia safari njema.
Baada ya maelezo hayo, Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 6:38 Mchana.

= UMETHIBITISHWA =

| | | |
|---|---|---|
| ........................ | 17/11/2021 | ........................ |
| **Katibu** | **Tarehe** | **Mwenyekiti** |